# WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
# CHUO CHA UALIMU KITANGALI

Barua pepe:
kitangali@gmail.com
kitangalitc@moe.go.tz
Simu +2550689793460

Chuo cha Ualimu
Kitangali
S. L. P. 75
Newala - Mtwara
30, Mei, 2025

# BARUA YA KUJIUNGA NA CHUO

## 2025-2026




| MOTO WA CHUO | MAISHA NI MAPAMBANO |
| --- | --- |

## UTANGULIZI

Ninakupongeza kwa kuchaguliwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kujiunga na Chuo cha Ualimu Kitangali kwa mafunzo ya Stashahada ya Ualimu wa Elimu ya Msingi katika masomo ya Hisabati na Sayansi mwaka wa masomo 2024/2025.

## CHUO MAHALI KILIPO

Chuo kipo Mkoa wa Mtwara Wilaya ya Newala Vijijini katika Uwanda wa Juu wa Makonde (Makonde Plateu). Umbali wa kilometa 160 kutoka Mtwara Mjini, Kilometa 40 kutoka Newala Mjini au Kilometa 40 kutoka Mtama Barabara kuu itokayo LINDI kwenda MASASI.

## NAMNA YA KUFIKA CHUONI

Ukitokea njia ya Dar es Salaam panda basi la ***Dar es Salaam - Newala*** Kupitia Kitangali chuoni ambayo ni, ***Mahuta Express au Ibra Expess, Zufaa Express nk.*** Tiketi zinapatikana ***Temeke Sudani na Mbagala Bus Terminal***. Ukitokea Songea kupitia Masasi panda basi la Lindi au Mtwara na ushuke Mtama. Ukiwa Mtama utapata usafiri wa kufika Kitangali chuoni.

## MAELEKEZO KUHUSU SHERIA NA TARATIBU ZA CHUO

i) Chuo kitafunguliwa tarehe **13/07/2025** mwisho wa kuripoti Chuoni ni tarehe **16/08/2025**, usipofika kwa tarehe hii nafasi yako utaipoteza na atapewa mtu mwingine.

ii) Kozi hii inatolewa kwa muda wa miaka miwili(2) kwa makundi yafuatayo:-

- Kundi la kwanza ni wale wanafunzi wanaojiendeleza (in-service teachers na waliohitimu kozi ya Astashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi)
- Kundi la pili ni wale waliohitimu mafunzo ya Sekondari ya juu(ACSEE) kupata ufaulu wa daraja la kwanza hadi la tatu( Division I-III).

iii) Ukishafika hapa chuoni utapewa sheria na taratibu za chuo ambapo ukishazisoma na kuzielewa utajaza fomu ya kukubaliana nazo.

**N.B.** Utakapofika chuoni nenda Idara ya Udahili, Mitihani na Utoaji vyeti kwa ajili uhakiki wa vyeti, Benki pay in slip na mahitaji mengine uliyoagizwa, kisha kusajiliwa.

Benki pay in slip ya Michango na fomu ya malipo (Control Namba) vipelekwe kwa mhasibu ili upewe risiti.

## MAHITAJI YA USAJILI

Ili Mwanachuo asajiliwe anatakiwa kuja na nyaraka zifuatazo:-

i) Barua ya kuitwa kujiunga na mafunzo ya Ualimu (Fomu itatumwa na chuo).

ii) Barua ya ruhusa kutoka kwa mwajili( inawahusu walimu wanaojiendeleza wakiwa kazini)

iii) Vyeti HALISI (Academic na Leaving certificate) vya kidato cha sita, cheti cha Astashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi kwa wanaojiendeleza pamoja na cheti cha kuzaliwa.

iv) Uje pia na vivuli (photocopies) vya vyeti vyako vyote.

v) Hakikisha umepimwa na **Daktari wa hospitali ya serikali** na kujaziwa fomu iliyo ambatanishwa kwenye barua hii kuthibitisha hali ya afya yako

## ADA YA CHUO

ADA ya mwaka ni Tshs 450,000/- ambayo unaweza kulipa kwa awamu mbili kwa mwaka yaani Tshs 225,000/= kwa muhula mmoja.

## MICHANGO MINGINE

i) Huduma ya kwanza Tshs 10,000/≈ kwa mwaka;
ii) Usajili na kitambulishoTshs 20,000/≈ inalipwa mara moja kwa mwaka wa kwanza
iii) Serikali ya wanachuo Tshs 5,000/≈ kwa mwaka;
iv) Kukodi godoro Tshs 10,000/≈ kwa mwaka;
v) Michezo Tshs 30,000/≈ kwa mwaka;
vi) Ulinzi Tshs 30,000/≈ kwa mwaka;
vii) Usafi na Mazingira Tshs 20,000/≈ kwa mwaka;
viii) Ukarabati Tshs 25,000/≈ kwa mwaka; Ada ya Mtihani wa Taifa (NECTA) Tshs 50,000/- (**Inalipwa mwaka wa II** )
ix) ***Ni lazima kila mmoja aje na BIMA ya afya kama anayo. Na kama hana BIMA ni lazima kulipa Tshs 50, 400/***

## NAMNA YA KUFANYA MALIPO YA ADA NA MICHANGO

i) Fedha ya ADA italipwa baada ya mwanachuo/mzazi/mlezi kuwasiliana na Mkuu wa Chuo/Mhasibu wa chuo na kupewa namba maalum ya mfumo wa malipo ya serikali (CONTROL NUMBER) ndipo ufanye malipo hayo.

ii) Fedha za MICHANGO YOTE zilipwe kwenye *Akaunti Namba 70803500041 JINA LA AKAUNTI: KITANGALI TTC –TEACHERS' TRAINING COLLEGE*. Akaunti hii ni ya NMB. Unaweza kulipa fedha hizo kwenye tawi lolote la NMB nchini.

iii) Uje na Bank pay in slip ya malipo hayo . Kumbuka kuandika jina lako kwenye Bank pay in slip unapoweka fedha benki . Fedha taslimu hazipokelewi chuoni na FEDHA IKISHALIPWA HAIRUDISHWI.

iv) Usipitishie fedha binafsi kwenye Akaunti ya Chuo.

**MUHIMU**

***Wazazi/Walezi ni lazima wawakatie watoto wao Bima ya Afya ya shilingi elfu hamsini mianne (sh.50, 400/=) kwa mwaka kurahisisha huduma za matibabu awapo chuoni na mahali popote Tanzania.***

## SARE ZA CHUO

### Wavulana

i) Suti nyeusi mbili (suruali ziwe za mshono wa heshima siyo za kubana). Angalia mchoro wa suruali na uzingatiwe.
ii) Mashati mawili ya mikono mirefu rangi ya light blue.
iii) Viatu vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi vya kufunika vitavaliwa na soksi
iv) Tai ndefu nyeusi nyeusi.




### Wasichana

i) Suti nyeusi jozi mbili zinazovuka magoti, sketi zenye mshono wa Λ kwa mbele. Angalia mchoro wa sketi na uzingatiwe.
ii) Mashati mawili ya mikono mirefu rangi ya light blue.
iii) Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunika vyenye visigino vifupi.
iv) Tai fupi nyeusi (siyo butterfly tie).
v) Soksi nyeupe ndefu.
vi) Watakaopenda kuvaa Hijab watumie rangi ya bluu bahari (ifanane na shati).

## MAVAZI MUHIMU KWA WOTE

i) Uje na bukta moja
ii) T-Shirt moja – sare ya chuo ( inapatikana chuoni kwa Tshs 15,000/= ).
iii) Njoo na track suit ya bluu au nyeusi.
iv) Njoo na raba za michezo.
v) Mavazi (mashono) mengine yote utakayokuja nayo nje ya sare yawe ya heshima na yanayoakisi haiba ya Ualimu.

## MAAGIZO YA VIFAA MUHIMU

i) Vyombo vya chakula – sahani, bakuli, kikombe ( visiwe vya plastiki), kijiko, galoni jeupe la lita 5 la kuhifadhia maji yako ya kunywa.
ii) Ndoo ya kuogea
iii) Tochi ya betri au solar kwa ajili ya

## MAHITAJI MUHIMU KWA AJILI YA MALAZI

i) Shuka mbili za bluu .
ii) Mto na foronya za bluu.
iii) Chandarua kwa ajili ya kujikinga na mbu.

## MAHITAJI MENGINE

Ili kuweza kujikimu kimaisha uwapo hapa chuoni kwa mahitaji madogomadogo unapaswa kuja na fedha za matumizi.

***N.B***

***Kumbuka kuja na sanduku imara lenye kufuli kwa utunzaji salama wa vifaa vyako.***

tahadhari ya kukosekana kwa umeme.

## TAALUMA

Chuo cha Ualimu Kitangali kinatoa kozi ya Stashaha ya Ualimu Elimu ya Msingi katika masomo ya hisabati na sayansi. Walimu hawa huimarishwa katika mahiri za pedagojia ya kufundishia na kujifunzia kama ilivyofafanuliwa katika mtaala ulioboreshwa wa kozi husika wa mwaka 2023.

Idara ya taaluma katika Chuo cha Ualimu Kitangali imejidhatiti kuhakikisha taaluma inayotolewa inamuandaa Mwalimu mahiri atakayeweza kufundisha Wanafunzi katika ngazi ya Elimu ya Msingi. Pia Chuo kimejikita katika kuhakikisha mhitimu wa Chuo cha Ualimu Kitangali anakuwa mwalimu mwenye weledi na umahiri wa kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji unaoendana na mabadiliko ya kisayansi, kiteknolojia na kijamii.

### Mwanachuo atahudumiwa na Ofisi zifuatazo:-

- Mkuu wa Chuo.
- Masuala ya taaluma.
- Masuala ya wanachuo.
- Huduma saidizi.

## MAHITAJI YA LAZIMA KWA AJILI YA TAALUMA

Ofisi ya masuala ya taaluma inashauri kila Mwanachuo kuja na vifaa vifuatavyo:-

i) Mathematical set 1.
ii) Daftari kubwa zisizopungua 11.
iii) Kamusi ya Kiswahili na Kamusi ya Kiingereza**.**
iv) Rimu moja ya karatasi A4 kwa mwaka.(N.B.Leta rimu siyo fedha).

## MABWENI

Chuo kina mabweni mazuri ya kisasa kwa Wanachuo wote, yenye huduma ya maji, umeme, maeneo ya kufulia na mandhari nzuri yenye bustani ya maua, miti, matunda na nyasi. Mabweni yanayotumiwa na wanachuo wa kike yana huduma zote muhimu kwa ajili yao.

## MICHEZO & BURUDANI

Chuo kinatoa fursa kwa kila Mwanachuo kushiriki michezo na kukuza kipaji chake. Katika ngazi ya Chuo Mwanachuo atashiriki mashindano ya michezo ngazi ya madarasa na mabweni kwa michezo yote ya mpira wa miguu, mpira wa mikono (hand ball), mpira wa kikapu (basketball), mpira wa pete (net ball), Volleyballs, na table tennis. Pia atashirki katika michezo ya riadha (mbio, miruko ya juu na chini), kurusha mkuki na tufe.

Vile vile Mwanachuo atapata fursa ya kushiriki michezo ya ndani ambayo hujumuisha mchezo wa bao, draft, maigizo, nyimbo, kuonesha vipaji katika maeneo ya kucheza ngoma, sarakasi, na kughani mashairi, pia atapata fursa ya kuonesho kibaji chake katika mitindo mbalimbali ya kitamaduni na kisasa.

Chuo cha Ualimu Kitangali ni miongoni mwa vyuo vinne vya Ualimu vinavyopatikana katika kanda ya kusini. Chuo kimekuwa kikishiriki katika mashindano ya michezo na taasisi jirani na kushiriki katika mashindano ya michezo ya vyuo nchini (UMISAVUTA).

## UHIFADHI WA MAZINGIRA (Green Mind Green Life)

Chuo cha Ualimu Kitangali kina mandhari nzuri ya kuvutia. Chuo kipo kwenye mwinuko wa Uwanda wa Juu wa Makonde kinapakana na mto unaotiririka kipindi chote cha mwaka pamoja na msitu wa asili. Chuo chetu kimezungukwa na miti ya asili na ya kupandwa. Wanajumuia wa Chuo wako mstari wa mbele kuhakikisha wanatunza na kupendezesha mazingira ya Chuo kwa kupanda maua na miti. Vilvile katika kukifanya Chuo kuwa sehemu bora kwa mafunzo na kivutio kimebuni bustani nzuri ya matunda na kukifanya chuo chenye mandhari murua kwa kupumzika. Vilevile Chuo kina shamba bora la mikorosho linalotoa fursa kwa wanachuo na wageni kujifunza kilimo cha zao la korosho.

**MWISHO:** **Mwalimu bora huandaliwa chuoni. Chuo cha Uwalimu Kitangali kimejidhatiti kukujenga kuwa mwalimu bora tangu mwanzo wa mafunzo yako hadi mwisho.**

**KARIBU SANA CHUO CHA UALIMU KITANGALI**

**MAISHA NI MAPAMBANO**

**NATHANAEL A. HINJU**

**MKUU WA CHUO**

**GOVERNMENT OF TANZANIA REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

From: KITANGALI
TEACHERRS'
COLLEGE, BOX 75 –
**NEWALA-**
**MTWARA.**

**STUDENT NAME**: ..........................................................................

**PART A:** TO the Medical Officer :
..........................................................................
..........................................................................

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full time teacherscourse.

A: 1. (a) Eye – sight:
(b) Hearing:
(c) Speech:
(d) Venereal Diseases:
(e) Leprosy:
(f) Limbs:
(g) Epilepsy:
2. Neuroses:
3. Other serious diseases:B: Blood Group:

Date: .........................            Signature........................... ..............................
Official Stamp

****************************************************************************

**PART B:**            **MEDICAL CERTIFICATE.**
(To be completed by Government Medical Officer)

I have examined the above named student that he/she is physically fit/unfit and mentally *fit/unfit fora full time teacher Education course.

(a) Eye – sight..............................................................
(b) Hearing.......................................................................
(c) Limbs......................................................................
(d) Speech.....................................................................
(e) Leprosy.......................................................................
II. Neuroses..........................................................................
III. Other serious diseases....................................................................
IV. Pregnancy..........................................................................

Blood Group: ....................................................................

**Date:**.........................  **Signature:** .................. **Official Stamp** ............................